




## Kukaa salama



### Katika hali ya dharura



Katika hali ya dharura, pigisa simu Sufuri Tatu (000).



Watakuuliza ikiwa unahitaji:

- ambulensi



- moto



- polisi



Wewe unahitajika kuwaambia huduma ngani ambayo unahitaji.



Pigia 000 pekee ikiwa kunayo hali ya **dharura**.



Kama huwezi kuzungumza Kiingereza, sema 'Mkalimani' na jina la lugha wewe unasema.




Waambie:

- jina lako




- anwani ambapo hali ya dharura ipo



- nambari yako ya simu



- nini kinachotokea



Kama wewe unachanganyikiwa na hawajui nini cha kusema, usikate.

Kukaa kwenye laini na mwenye simu anaweza kugundua ambapo upo wapi unapopigia simu na kutuma msaada.



**Huduma za ambulansi ni kwa ajili ya hali ya dharura tu.**

**\$\$\$**

Wewe unaweza kulipa kutumia ambulensi ikiwa huna:

- bima ya afya ya kibinafsi
- kadi ya huduma ya utunzaji wa afya
- kadi ya konsesheni



# Kukaa na usalama nyumbani

## Maji



Ni salama kuyatumia maji kutoka kwenye bomba kwa ajili ya:


- kunywa
- kupika



Usinywe au kutumia maji kutoka ziwa, mto au mito – maji hayo yanaweza kuwa machafu au hatari.



Maji ya moto yanaweza kukuchoma wewe.




Ni muhimu kuangalia jinsi maji yapo moto kabla:

- kuingia ndani ya bafu ya kuogea
- kuingia katika bafu
- kuwaweka watoto kwenye maji


## Umeme




Mshtuko wa umeme unaweza kuumiza na hata kuuu watu.



Usitende:




- kuweka vifaa vya umeme karibu na shimo au chanzo kingine chochote cha maji




- kuweka vitu vya chuma katika
  - toaster



- microwave



- hatua ya nguvu




Juu ya jiko na tanuri zinakuwa moto sana.

Wakati wewe unapokuwa unapika, weka sehemu ya kushikia sufuria kama imegeuka ili watoto wasiweze kuifikia.



Weka watoto mbali na mlango wa tanuri – inaweza kuwa moto sana.

## Gesi



Gesi hutumika katika:

- vito vya jiko




- tanuri




- mashine ya joto



Zima tanuri ya gesi au jiko wakati kumaliza kutumia.



Ikiwa wewe unainusa harufu ya gesi, basi usiwashe kibiriti – moto unaweza kufanya gesi ikalipuka.



Tafuta wapi uvujaji wa gesi unatoka.

Zima gesi moja kwa moja.


## Dawa na kemikali




Madawa pamoja na kemikali fulani ambazo watu huhifadhi nyumbani zinaweza kuumiza watu au kuwafanya watu wakagonjeka sana.



Weka madawa yote mahali ambapo watoto hawawezi:



- kufikia
- kuyapata



Weka bidhaa zote za kusafisha kwenye kabati iliyofungwa na kufuli, mahali ambapo watoto hawawezi kufikia.

## Chakula



Karibu nyumba zote za Australia zina friji ya kuweka chakula safi.


Mara nyingi huitwa friji.





Chakula fulani huhitajika kuhifadhiwa kwenye friji mpaka utakapo kuwa tayari kukitumia:


- bidhaa za maziwa – maziwa, siagi, krimu, jibini




- nyama, samaki na dagaa



- matunda na mboga fulani




Vyakula vingine vinapaswa kuhifadhiwa barafuni vyema mpaka utakayokwisha kupika.



Friji nyingi zinazo sehemu maalum kwa ajili ya kufungia chakula.

Hii inaitwa friza.



Baadhi ya nyumba nchini Australia huwa na friza tu kwa ajili ya vyakula vilivyohifadhiwa.



Wewe unapaswa kufungia chakula kwenye friza mara moja tu.

Inaweza kukufanya wewe ukagonjeka ikiwa wewe unakula chakula kilichohifadhiwa kwenye friza kwa zaidi ya mara moja.



Osha matunda pamoja na mboga zako kabla ya kula.

Hii itaondoa kemikali ambazo zimetumika kuwalinda kutokana na wadudu.



Weka safi maeneo yako yote ya kupikia.



Hakikisha kuwa kila mara unanawa mikono yako kabla ya kukula chakula.

## Moto



Kilio cha alamu ya moshi lazima kutumika katika nyumba zote.



Alamu ya moshi hufanya kilele kubwa ikiwa kuna moshi.



Alamu ya moshi hutumia betri.

Betri inapaswa kupimwa pamoja na kubadilishwa kila baada ya miezi 6.



Uangalifu sana na mishumaa au sigara.

Hiyo ni sababu ya kawaida ya moto wa nyumba.



Usiweke nguo karibu au juu kwenye mashine ya kupasha joto.



Tengeneza mpango wa jinsi ungetoka nyumbani kwako ikiwa kuna moto.

Fanya mazoezi na mpango wa uokoaji na jamii yako.

## Kukaa salama barabarani


### Kuvuka barabara



Nchini Australia magari huendesha kwenye upande wa kushoto wa barabara.



Wakati unapovuka barabara, angalia kwa makini upande wako wa kushoto na kulia ili kuchunguza trafiki.



Ivuke barabara katika:

- mataa ya trafiki
- kivuko cha wenda wa miguu

## Kuendesha baiskeli




Lazima uvae kofia ya chuma wakati unapopanda baiskeli.



Katika Australia, baiskeli mara nyingi huitwa bikes.

Watu wanaoendesha baiskeli wanaitwa wapandabaiskeli.



Wapanda baiskeli lazima watii sheria zote za barabara.



Wewe huna haja ya leseni ya kupanda baiskeli kwenye barabara.



Wewe unahitaji kufuata sheria sawa za kuendesha gari.



Ikiwa wewe unaendesha wakati wa usiku, baiskeli yako lazima iwe na:

- taa la mbele
- taa la nyuma




Miji mingi ina njia maalum za kuendeshea baiskeli ambazo waendeshaaji baiskeli wanaweza kutumia.

## Madawa ya kulevya na pombe



Ni hatari na nje ya sheria kuendesha gari ikiwa wewe umetumia madawa ya kulevya au kunywa pombe.




Ikiwa wewe umekamatwa ukiendesha gari baada ya kunywa pombe au kutumia madawa ya kulevya, wewe unaweza:

- kupewa faini – kulipishwa kiasi kikubwa cha pesa



- kupata leseni yako kuondoa kwako



- kufungwa jela

Ukurasa huu umewachwa tupu makusudi



**Australian Government**  
**Department of Social Services**

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji  
la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya  
Huduma za Jamii nchini Australia

